**Mpango wa Elimu kwa Wahamiaji wa Pennsylvania**

# Zana za Mradi wa Diploma

---

**Mwongozo wa Wazazi wa Pennsylvania: Mkakati wa Chuo cha elimu na Kazi**

***Oktoba 2018*** *(Imerekebishwa)*

**JUMUIYA YA MADOLA YA IDARA YA ELIMU YA PENNSYLVANIA**
333 Market Street
Harrisburg, PA 17126-0333
www.education.pa.gov

**Jumuiya ya Madola ya Pennsylvania**
Tom Wolf, Gavana

**Idara ya Elimu**
Pedro A. Rivera, Katibu

**Ofisi ya Elimu ya Chekechea/Sekondari**
Matthew Stem, Naibu Katibu

**Ofisi ya Usaidizi wa Shule**
Sherri Smith, Mkurugenzi

**Divisheni ya Huduma za Wanafunzi**
Carmen Medina, Mkuu

Idara ya Elimu ya Pennslyvania (PDE) haibagui katika mipango yake ya elimu, shughuli, au ajira, kwa misingi ya umbari, rangi, asili ya kitaifa, jinsia, mwelekeo wa jinsia, ulemavu, umri, dini, ukoo, uanachama wa uanachama wa muungano, utambulisho wa kijinsia, hali ya Ukimwi au HIV, au kategoria nyingine yoyote inayolindwa na sheria. Tangazo la sera hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Serikali ikiwemo Sheria ya Mahusiano ya Binadamu ya Pennsylvania na pamoja na Sheria ya Shirikisho, ikiwemo Kichwa cha VI na Kichwa cha VII cha Sheria ya 1964 ya Haki za Raia, Kichwa cha IX cha Marekebisho ya Elimu ya 1972, Sehemu ya 504 ya Sheria ya 1973 ya Urekebishaji tabia, Ubaguzi wa Umri katika Sheria ya Ajira ya 1967, Sheria ya 1990 ya Wamerikani wenye Ulemavu.

Watu wafuatao wamechaguliwa kushughulikia maswali yanayohusu sera za kutobagua za Idara ya Elimu ya Pennsylvania:

**Kwa Maswali Kuhusu Kutobagua katika Ajira:**
Idara ya Elimu ya Pennsylvania
Mwakilishi wa Nafasi Sawa za Ajira, Ofisi ya
Rasilimali Watu
Simu: (717) 783-5446

**Kwa Maswali Kuhusu Kutobagua katika Mipango na Shughuli Zingine Zozote za Idara ya Elimu ya Pennsylvania:**
Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za
Shule, Idara ya Elimu ya Pennsylvania
333 Market Street, Gorofa ya 7, Harrisburg, PA 17126-
0333 Simu: (717) 783-3750, Faksi: (717) 783-6802

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu chapisho hili au kwa makala ya ziada, wasiliana na:

Pennsylvania Department of Education
Bureau of School Support | Division of Student Services
333 Market Street, 3rd Floor, Harrisburg, PA 17126-0333
Voice: (717) 783-6466, Faksi: (717) 783-6642
www.education.pa.gov

Maombi/Maswali yote ya Vyombo vya Habari: Wasiliana na Ofisi ya Waandishi wa Habari na Mawasiliano katika (717) 783-9802.

# Ukurasa wa Yaliyomo


Kitengo cha Wazazi – Mkakati wa Chuo cha Elimu na Kazi ........................................................4
Kuweka Malengo ..........................................................................................................................5
Mpango wa Wazazi na Wanafunzi ................................................................................................6
Utathmini wa Kibinafsi wa Wazazi .................................................................................................8
Timu ya Usaidizi..............................................................................................................................9
Sifa za Shule ya Sekondari ...........................................................................................................12
Mitihani na Mikakati ya Kufanya Mtihani.......................................................................................14
Kupangia Elimu ya Baada ya Sekondari .......................................................................................17
Mipango ya Baada ya Sekondari ..................................................................................................18
Kulipia Elimu ya Baada ya Sekondari............................................................................................22
Vidokezo na Rasilimali za Ziada ...................................................................................................26

# Kitengo cha Wazazi – Mkakati wa Chuo cha Elimu na Kazi

## Kitengo kwa Mtazamo wa Haraka

Hiki ni kitengo cha kipekee kwa ajili ya wazazi na walezi. Kinashirikisha vipengele kutoka kwa kila kitengo kwa ajili ya wanafunzi. Muundo ni rahisi kutumiwa na wazazi na wazi. Nyenzo inapaswa kushughulikiwa katika warsha mbili au zaidi.

## Mambo muhimu

- Kuweka malengo na mpango wa wazazi na wanafunzi
- Timu ya usaidizi
- Sifa za Shule ya Sekondari
- Mikakati ya kufanya mtihani
- Orodha ya ukaguzi ya mipango ya baada ya sekondari

### Ninawezaje kuwa wa msaada?

Fikiria kuhusu uwezo, vipaji, na raghba ambayo daima umeona katika mtoto wako na upendekeze ajumuishe katika kuendeleza wasifu wa kazi.

Tengeneza orodha ya marafiki, washiriki, wanafamilia, au wanajumuiya watatu au wanne ambao wanaweza kuzungumza na mtoto wako kuhusu chaguo za kazi.

Uliza mtoto wako kuhusu shughuli za ziada ambazo zinaweza kumsaidia kukuza kipaji, ujuzi, au raghba.

Himiza mtoto wako kuendelea na shule.

Sikiliza, sikiliza, sikiliza!

Msaidie mtoto wako kufanya kazi kupitia mchakato badala ya kubishana dhidi ya mawazo ambayo hukubaliani.

Unafahamu zaidi kile kinachomtia motisha mtoto wako—tabasamu, kichekesho, kumbatio—ikiwa amekata tamaa au kulemewa.

# Kuweka Malengo

## Ninawezaje kuunga mkono chaguo la mtoto wangu yla kazi?

Kama watu wanaofahamu mtoto vizuri, wazazi na walezi wako katika nafasi ya kipekee na ya thamana ya kutoa maoni na maelezo. Wazazi na walezi wengi wana wasiwasi kuhusu chaguo la mtoto wao la mkakati wa kazi, hata kama wanafurahi kwamba mtoto wao anatambua kile angependa kufanya maishani. Kwa hiyo, unapaswa kuweka malengo kwa ajili ya mtoto wako.

### Kuweka Malengo

- **Fanya kuweka malengo iwe ya kuhusisha iwezekanavyo –** Sisi wote tunataka kilicho bora kwa watoto wetu. Fundisha mtoto wako kufikiria kuhusu kuweka na kufikia malengo. Hii itamsadia kukuwa chanzo chao bora cha utekelezaji. Hii itamwezesha kudhibiti matokeo katika maisha yake na kumpa utambuzi aonastahili.

- **Weka malengo ya muda mfupi na ya muda mrefu** – Kuweka malengo inaweza kuwa na manufaa au madhara. Malengo ya muda mfupi na ya muda mrefu yanafaa kuwa rahisi, yenye uhalisi, na yanayowezekana. Shirikiana na mtoto wako kugawanya malengo ya muda mrefu kuwa hatua zinazowezekana. Kwa mfano:
    - Lengo la muda mrefu la kuboresha Kiingereza chao linaweza kuwa na malengo ya muda mfupi kama vile, kujifunza maneno mapya matatu na dhana yao kila wiki.  Hii itasaidia kujenga msamiati wao wa kitaaluma.

- **Tambua uwezo na udhaifu –** Hisia ya furaha mtoto wako anapata kutokana na kufikia malengo madogo, lakini yenye maana yatasaidia kuimarisha nguvu na imani anapoelekea kwenye mafanikio makubwa. Msaidie kujifunza faida za kuweka malengo madogo, yanayowezekana, na ya muda mfupi.

- **Tambua rasilimali zilizopo katika shule na jumuiya –** Fikiria kuhusu rasilimali zilizopo wakati mtoto wako anaongea mara ya kwanza kuhusu kuvunjwa moyo, masikitiko, na kutojiweza shuleni.
    - Ninaweza kufanya nini kama mzazi ili kusaidia mtoto wako kuhitimu kutoka shule ya sekondari?
    - Nani anayeweza kunisaidia?
    - Ninafahamu matakwa ya kuhitimu shule ya sekondari?
    - Ni changamoto gani zinazonizuia kumsaidia mtoto wangu?

****Jiskie huru kuomba usaidizi kutoka kwa Mtaalamu wa Usaidizi wa Mwanafunzi wako wakati unapanga malengo.

## Mpango wa Wazazi na Wanafunzi

Chati iliyo hapa chini inachunguza malengo ya shule, malengo ya mtoto wako, na malengo yako kama mzazi. Baada ya kuorodhesha malengo, unda mpango wa kuyatimiza, onyesha ikiwa ni ya muda mrefu au mfupi, na weka tarehe ya lengo. Hii anapaswa kuwa mwanzo wa mazungumzo mazuri kati ya wewe na mtoto wako.

| Malengo | Panga kutimiza lengo langu (k.v. Masomo au shughuli zinazohitajika) | Ya muda mrefu au mfupi? | Tarehe ya Lengo |
|---|---|---|---|
| Shule | | | |
| Mwanafunzi | | | |
| Mzazi | | | |

**Wasiwasi wangu ni?**

Mtoto wangu anaweza kufanikiwa katika kazi hii?

Mtoto wangu ana ujuzi na ufahamu unaohitajika kwa ajili ya aina hii ya

kazi? Mtoto wangu ataendelea na uamuzi wake?

Mtoto wangu anaweza kujisaidia kwa kufanya aina hii ya kazi?

Je, njia hii ya kazi itahitaji mtoto wangu kuondoka kwenye jumuiya yetu ili kwenda kusoma na kufanya kazi?

Ni matarajio gani ya muda mrefu ya kazi hii?

**Kidokezo cha Wazazi**

Mawasiliano ni "ya pande mbili." Wanafunzi wanaweza kuleta maelezo muhimu kutoka shuleni na kutoka kwa washauri! Wazazi, wakiwemo wale ambao hawajakuwa kwenye shule ya sekondari au chuo kikuu, wanaweza kutoa ushauri!

# Utathmini wa Kibinafsi wa Wazazi

Kama wazazi, mnafanya kazi muhimu katika "timu ya upangaji" ya mtoto wako. Anza kwa kuweka jukumu lenye manufaa, la kuunga mkono ili kuhakikisha kuwa mtoto wako ana kila kitu kinachohitajika kukamilisha shule ya sekondari. Shirikiana na mtoto wako na shule ili kutambua hatua ambazo zitasababisha kazi ya kuridhisha na elimu ya chuo kikuu zaidi ya kuhitimu shule ya upili. Tumia orodha hii ya kukagua ili kubainisha jinsi unavyoendelea katika maeneo haya:

## Uwezo

- ☐ Ninaamini kwamba mtoto wangu anaweza kufanya kazi bora sana katika masomo yake.
- ☐ Ninafanya kazi kama timu na mtoto wangu, na ninashiriki katika mchakato wa kukusanya maelezo ambayo mtoto wangu anahitaji.
- ☐ Niko tayari kuwa kama mfano wa kufanya kazi kwa bidii, kujitegemea, na ushupavu kwa ajili ya mtoto wangu.
- ☐ Ninazungumza na mtoto wangu mara nyingi kuhusu mipango yake ya baadaye, na husikiliza maoni na mipango yao.


## Changamoto

- ☐ Ninashuguli kazini na daima sina wakati wa mazungumzo na mtoto wangu.
- ☐ Mtoto wangu ni wa kwanza katika familia kuwa na lengo la kuenda chuo kikuu.
- ☐ Wakati mwingine husita na sijui nitapata usaidizi wapi.
- ☐ Sina uhakika ni kozi gani ambazo mtoto wangu anahitaji kufanya ili kuhitimu kutoka shule ya sekondari.
- ☐ Ninafahamu raghba na mapendeleo ya mtoto wangu.
- ☐ Ninafahamu mipango ya mtoto wangu ya chuo kikuu/kazi baada ya shule ya sekondari.

## Kupanga Mapema

- ☐ Niko tayari kujitolea kiuchumi ili kumsaidia mtoto wangu kufanikiwa shuleni.
- ☐ Nitahitaji/nitatafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya elimu ya baada ya sekondari ya mtoot wangu na kuwa na mpango wa kuweka akiba.
- ☐ Ninafanya kazi ya kuratibu ratiba ya familia yangu ili kuunga mkono ratiba ya mtoto wangu ya kitaaluma.

- ☐ Ninaweza kumsaidia mtoto wangu na mwongozo wa kupata au kutunza kazi.
- ☐ Ninaunga mkono raghba au malengo ya mtoto wangu.
- ☐ Ninafahamu na nimejitayarisha kusaidia usafiri wa mtoto wangu na mipango ya kuishi baada ya shule ya sekondari.




## Timu ya Usaidizi

**Umuhimu wa kuunda timu ya usaidizi kwa ajili ya wazazi**
Ni muhimu sana kwa wazazi wahamiaji kufahamu na kuunga mkono siku za baadaye za watoto wao kwa kufikia mashirika ya kijamii, maktaba, vituo vya burudani, na mashirika ya kidini ambayo wanashiriki. Wanaweza kutoa msaada wa kitaaluma au shughuli za burudani. Haya ni mambo muhimu kwa mafanikio ya kitaaluma. Majukumu ya mzazi na walimu au watu wa usaidizi hayawezi kubadilishwa, lakini badala yake kusaidia na kuimarisha majukumu ya kila mmoja ili kuhakikisha mafanikio ya mtoto. Wazazi wanahitaji kuchukua hatua ya kuhudhuria na kuunga mkono shughuli zote ambazo watoto wao hushiriki ili kusaidia watoto wao kufanikiwa katika malengo ya muda mfupi na ya muda mrefu. Wazazi, walimu, na watetezi wanahitaji kujenga ushirikiano ili kuunda jitihada zinazoendelea kwa lengo la pamoja: kuona watoto wao wakifanikiwa.

## Timu ya Usaidizi ya Wazazi

| Msaada wa Lugha | Shule | Mashirika ya Kijamii | Maktaba | Vituo vya Burudani | Mashirika ya Kidini | Wanafamilia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Shule zote zinapaswa kuwa na simu ya msaada wa lugha. | Wajue walimu, washauri, mkuu wa wanafunzi na wafanyakazi wa usaidizi wa mtoto wako. | Toleo katika jumuiya yako ni nini? | Aina gani ya shughuli au warsha za elimu ambazo inatoa? | Aina gani ya michezo au shughuli za burudani ambazo inatoa? | Aina gani ya huduma ambazo inatoa ili kusaidia mtoto wangu? | Ninaweza kutegemea mwanafamilia huyu kusaidia kuwahamasisha watoto wangu kupitia viwango vyao vya elimu. |
| Ni nani anayefaa kwa usaidizi huu? | | | | | | |

# Timu ya Usaidizi ya Wazazi

| Msaada wa Lugha | Shule | Mashirika ya Kindani ya Jumuiya | Maktaba, Vituo vya Burudani, Mashirika ya Kidini | Mitandao Mingine ya Msaada ya Washauri |
|---|---|---|---|---|
| Simu ________________<br><br>Lugha______________<br><br>Kwa sheria, wilaya ya shule lazima watoe msaada kwa wanenaji wa lugha zingine. Wazazi wanahitaji kuwapata wakalimani ili kushiriki katika mkutano au shughuli yoyote ya shule. Hii inajumuisha mkutano na walimu, washauri, mkuu wa wanafunzi, wasaidizi wa shuleni. | **Walimu**<br><br>Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________<br><br>**Mshauri**<br><br>Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________<br><br>**Mkuu wa Shule/Mkuu wa Wanafunzi**<br><br>Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________<br><br>**Mfanyakazi Mhamiaji**<br><br>Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________ | **Waratibu**<br><br>Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________<br><br>**Wahudumu wa Kesi**<br><br>J Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________<br><br>**Viongozi wa Timu**<br><br>Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________ | **Waangalizi wa maktaba**<br><br>Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________<br><br>**Viongozi wa Mpango**<br><br>Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________<br><br>**Mpango unaanza lini?**<br><br>_______________________<br><br>_______________________<br><br>_______________________<br><br>_______________________<br><br>_______________________<br><br>_______________________ | Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________<br><br>Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________<br><br>Jina ____________________________<br><br>Simu ____________________________<br><br>Barua pepe ____________________ |

Nchini Marekani, wazazi hukutana na walimu, washauri wa shule, na wafanyakazi wengine wa msaada (kama vile wafanyakazi wa PA- MEP) ili kujadiliana kuhusu siku za baadaye za watoto wao.

Weka jina na maelezo ya mawasiliano ya mshauri wa shule ya mtoto wako, mwalimu aliyeaminika, mfanyakazi wa PA- MEP, na mshauri wa mtoto wako mahali pazuri na uwasiliane nao wakati unahitaji ushauri au msaada.

Nchini Marekani, watoto wanaweza kutokubaliana kwa heshima na wazazi wao. Ikiwa wewe na mtoto wako hamwezi kutatua suala, wasiliana na mshauri wa shule, mwalimu aliyeaminika, au mshauri wa mtoto kwa ajili ya suluhisho.

Kumbuka kuwasiliana na "timu yako ya kupanga" ili kusherehekea mafanikio, pia!

## Vyeti vya Shule ya Sekondari

Kila shule ina matakwa tofauti ya kuhitimu. Hapa chini ni mfano wa shule ya kawaida ya sekondari ya Pennsylvania. Orodha ya mtoto wako ya matakwa ya kozi itaonekana kuwa sawa na hii lakini hakikisha umejua matakwa halisi ya shule, ili mtoto wako aweze kufikia matakwa yote kikamilifu na kwa wakati unaofaa. Ikiwa huna ufikiaji rahisi wa maelezo haya kupitia tovuti ya shule yako, panga miadi na mshauri wa shule. Mshauri ndiye mtu mzuri wa kuomba maelezo haya.

| Masomo | Darasa la 9 | Darasa la 10 | Darasa la 11 | Darasa la 12 | Sifa |
|---|---|---|---|---|---|
| Kiingereza | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 |
| Hisabati | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 |
| Sayansi | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 |
| Sayansi ya Jamii | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 |
| Lugha ya Kigeni | | | 1 | 1 | 2 |
| Ubinadamu | 1 | 1 | | | 2 |
| Ya hiari | | | 1 | 1 | 2 |
| Afya na Elimu ya Kimwili | .5 | .5 | .5 | | 1.5 |
| Matakwa mengine ya Kuhitimu: Mradi wa Kuhitimu, Saa za Huduma na Mtihani wa Keystone | | | | **Jumla** | **23.5** |

Tafadhali jaza chati hapa chini pamoja na matakwa ya wilaya ya shule ya mtoto wako:

| **Masomo** | **Darasa la 9** | **Darasa la 10** | **Darasa la 11** | **Darasa la 12** | **Sifa** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kiingereza | | | | | |
| Hisabati | | | | | |
| Sayansi | | | | | |
| Sayansi ya Jamii | | | | | |
| Lugha ya Kigeni | | | | | |
| Ubinadamu | | | | | |
| Ya hiari | | | | | |
| Afya na Elimu ya Kimwili | | | | | |
| Matakwa mengine ya Kuhitimu: Mradi wa Kuhitimu, Saa za Huduma na Mtihani wa Keystone | | | | **Jumla** | |

Ikiwa mtoto wako ana shida na sifa, kuna rasilimali katika jumuiya, shule, serikali na mipango ya shirikisho na pia Mpango wa Elimu kwa Wahamiaji wa Pennsylvania. Zungumza na Mtaalamu wa Usaidizi wa Mwanafunzi Mhamiaji kuhusu mahali pa kupata rasilimali hizi katika jumuiya yako.

**Je, wajua?**

Katika Pennslyvania, watoto wana haki ya kupokea elimu ya umma bila malipo hadi wafikie umri wa miaka 21 - pasipo kutia maanani hali ya uhamiaji, afya, au uwezo wa utambuzi au kimwili.

## Mitihani na Mikakati ya Kufanya Mtihani

Chati kwenye ukurasa unaofuata huorodhesha mitihani iliyotolewa kwa madhumuni ya elimu zaidi ya shule ya sekondari/kazi na mitihani iliyodhaminiwa na serikali, kama vile mitihani ya Keystone:

## Mitihani ya Ukaguzi ya Hiari ya Gredi ya 11 na 12

| MITIHANI | PSAT<br><br>Mtihani wa Ukaguzi wa Masomo ya Utangulizi | SAT<br><br>Mtihani wa Utathmini wa Masomo | ACT<br><br>Mtihani wa Chuo Kikuu cha Amerika | TOFEL<br><br>Mtihani wa Kiingereza kama Lugha ya Kigeni | ASVAB<br><br>Mtihani wa Kukubaliwa Katika Kikosi cha Wanajeshi |
|---|---|---|---|---|---|
| Gredi | 11 | 11 na 12 | 11 na 12 | 12 | 12 |
| Gharama ya Mtihani | $16 | $45 Hakuna insha<br>$60 Insha | $62 | $195 | Hakuna Gharama |
| Tarehe za Mtihani | Majira ya baridi | Majira ya majani kupukutika | Majira ya baridi | Majira ya baridi | Itabainishwa |
| | Majira ya kuchipua | Majira ya baridi | Majira ya kuchipua | Majira ya kuchipua | na Anayewasajili |
| | Majira ya joto | Majira ya<br>Majira ya joto | Majira ya joto | | Wanajeshi |
| Maudhui ya Mtihani | Hesabu | Usomaji | Kiingereza | Kuzungumza | Hesabu |
| | Usomaji Muhimu | Kuandika | Hesabu | Kuandika | Sayansi |
| | Kuandika | Hesabu | Usomaji | Usomaji | Usomaji |
| | | | Sayansi | Kusikiliza | Elektroniki |
| | | | | | Ya Kiufundi |
| Madhumuni ya Mtihani | Hutoa maandalizi kwa ajili ya SAT na kutumika kuhitimu wanafunzi kwa Mashindano ya National Merit | Hupima hali ya kuwa tayari kwa chuo kikuu | Hupima hali ya kuwa tayari kwa chuo kikuu | Hutathmini ujuzi wa lugha | Hubainisha uainishaji wa kazi / nafasi kwenye jeshi |

## Utathmini Uliodhaminiwa na Shule

| MITIHANI | PSSA<br><br>Utathmini wa Kiwango cha Jimbo la PA | KEYSTONES | Mtihani wa WIDA ACCESS |
|---|---|---|---|
| Gredi | 3 - 8 | 11 | K-12 |
| Gharama ya Mtihani | Hakuna gharama | Hakuna Gharama | Hakuna Gharama |
| Tarehe za Mtihani | Aprili | Desemba, Januari, Mei | Majira ya baridi |
| Maudhui ya Mtihani | Hesabu<br>Kiingereza- Sayansi ya Sanaa ya lugha | Fasihi Biolojia Aljebra 1 Utungaji wa Kiingereza | Kusikiliza Kuzungumza Kusoma Kuandika |
| Madhumuni ya Mtihani | Kupima mafanikio ya mwanafunzi katika viwango vya serikali | Utathmini wa mwisho wa kazi uliyoundwa kushughulikia ustadi | Kubainisha Ukaguzi wa ESL |

Ifuatayo ni kigezo cha kalenda ambacho unaweza kutumia kurekodi tarehe za mtihani wa mtoto wako.

| SUNDAY | MONDAY | TUESDAY | WEDNESDAY | THURSDAY | FRIDAY | SATURDAY |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |

Andika kile utafanya pamoja na mtoto wako ili kuhakikisha wamefanikiwa katika mitihani yao.

| |
|---|
| Kabla ya Mtihani: |
| Baada ya Mtihani: |

## Kupangia Elimu ya Baada ya Sekondari

Sehemu hii inasisitiza hatua ambazo wazazi watahitaji kuchukua ili kujiandaa kwa ajili ya elimu ya baada ya sekondari. Majadiliano na maandalizi haya yanafaa kuanza mapema na kuhusisha walimu, washauri, wanafamilia na wanarika wengi iwezekanavyo.

**Ni aina gani ya shule/mpango wa elimu ya baada ya sekondari ambayo inalingana na vipaji na raghba za mtoto wangu?**

- Wazazi wanapaswa kuanza majadiliano na watoto wao kuhusu chaguo za baada ya sekondari wakiwa katika darasa la 8 au 9.
- Kila chuo, shule ya ufundi, na chuo kikuu nchini Marekani, kina matakwa yake yenyewe ya kuingia. Wazazi wanaweza kupata maelezo haya mtandaoni au kupitia mshauri wa shule au Mfanyakazi wa Msaada wa Mhamiaji.
- Wazazi wanapaswa kuwaunga mkono watoto wao kwa kujihusisha katika mipango iliyopo ya maandalizi ya chuo katika wilaya yoyote ya shule.

## Mipango ya Elimu ya Baada ya Sekondari

| Aina ya Chuo | Kile Unaweza Kupata | Mifano ya Kazi | Sifa |
|---|---|---|---|
| **Uanagenzi/Mafunzo ya Kazi** | ☐ Hati ya utambulisho iliyotambulika kitaifa kutoka kwa Idara ya Kazi ya Marekani<br>☐ Kazi ya Kulipwa<br>☐ Sifa za Chuo cha Elimu Bila Madeni<br>☐ Ufahamu na stadi zinazofaa maeneo ya kazi | ☐ Msanidi Programu<br>☐ Fundisanifu wa Duka la Dawa Makanika<br>☐ Msaidizi wa Uuguzi Aliyehitimu<br>☐ Mfanyakazi wa Ufundi wa Ujenzi<br>☐ Fundi wa meme<br>☐ Mtia weko | ☐ Kufanya kazi kuanzia siku ya kwanza<br>☐ Kuongezeka kwa Mishaharaka<br>☐ Mishahara ya ushindani katika maishani |
| **Shule ya Ufundi** | ☐ Cheti Diploma<br>☐ Shahada ya<br>☐ Chuo | ☐ Mtaalamu wa Programu za Kompyuta<br>☐ Mtaalamu wa Vipodozi<br>☐ Msaidizi wa daktari wa meno<br>☐ Mekanika<br>☐ Msaidizi wa Matibabu<br>☐ Fundi wa bomba | ☐ Madarasa madogo kwa ukubwa<br>☐ Madarasa ya jioni na wikiendi hutolewa<br>☐ Kuzingatia ujuzi muhimu kwa kazi maalum |
| **Chuo cha Jumuiya** | ☐ Cheti Diploma<br>☐ Shahada ya<br>☐ Chuo<br>☐ Uwezo wa kuhamisha kwa<br>☐ chuo au chuo kikuu cha miaka 4 | ☐ Mhasibu Mekanika wa Ndege Msaidizi wa Kisheria<br>☐ Mhudumu wa Hali za<br>☐ Dharura<br>☐ Mtaalamu wa Afya ya<br>☐ Meno Msimamizi wa<br>☐ Mkahawa | ☐ Madarasa madogo kwa ukubwa<br>☐ Madarasa ya jioni na wikiendi hutolewa<br>☐ Mara nyingi anaweza kuhama kwa chuo au chuo kikuu cha miaka 4<br>☐ Mara nyingi shule ndogo zinazopatikana katika jumuiya |
| **Chuo cha elimu au chuo kikuu cha miaka 4** | ☐ Shahada ya kwanza<br>☐ Shahada ya pili<br>☐ Shahada ya udaktari<br>☐ Shahada ya weledi | ☐ Mhandisi<br>☐ Wachoraji wa Picha<br>☐ Mfamasi<br>☐ Rubani<br>☐ Mfanyakazi wa<br>☐ Kijamii | ☐ Watu wengi uhudhuria wakati wote<br>☐ Anaweza kuchukua madarasa mengi tofauti<br>☐ Kwa kawaida huwa na bweni kwenye chuo |

## Maneno msingi

**Shahada ya chuo:** Aina ya shahada iliyotolewa kwa wanafunzi katika chuo cha Jumuiya cha Marekani, kwa kawaida baada ya miaka miwili ya masomo.

**Shahada ya kwanza:** Shahada iliyotolewa kwa mwanafunzi wa chuo kikuu, kwa kawaida baada ya miaka minne ya masomo katika chuo kikuu.

**Kazi:** Kazi ambayo wewe au mtoto wako amefundishwa.

**Chuo cha elimu:** Elimu yoyote baada ya shule ya sekondari ambayo inamwezesha mtoto wako kupata shahada.

**Chuo cha Jumuiya:** Vyuo vinavyotoa miaka miwili ya kwanza ya elimu ya chuo cha miaka minne au kuandaa wanafunzi kwa kazi fulani.

**Shahada:** Kile mtoto wako anapata wakati anahitimu kutoka chuo, kama vile shahada ya chuo au ya kwanza.

**Chuo cha Kiufundi:** Vyuo ambavyo hutoa masomo na mipango ya ajira, ambavyo hufundisha ufahamu na ujuzi maalum unaosababisha kupata kazi fulani.

**Chuo Kikuu:** Aina ya shule ambayo hutoa shahada na aina mbalimbali za masomo. Maombi ya kuruhusiwa kutolipa karo yanapatikana kwa wanafunzi wanaohitaji, kupitia washauri wa shule.

## Vipengele vitano muhimu vya insha nzuri ambavyo wazazi wanahitaji kufahamu

1. Kujihusisha katika shughuli za jumuiya na shule itatoa tajriba ambayo itawezesha mchakato wa kuandika insha.
2. Kutokuwa na isha kunaweza kuchelewesha mchakato wa maombi.
3. Mfanye mwalimu kupitia insha ya mtoto wako kabla ya kuwasilisha.
4. Msaidie mtoto wako katika mchakato wa kuandika insha na uwe katika mazingira mazuri.
5. Fuatilia maendeleo ya mtoto wako na uwaulize kuhusu njia za ziada ambazo unaweza kuwasaidia.

## Maandalizi kwa ajili ya Elimu ya Baada ya Sekondari

## Orodha ya Ukaguzi ya Mzazi

**Darasa la 9**

- ☐ Panga mkutano na mshauri wa shule ya mtoto wako ili kuhakikisha anafuata ratiba ili kuthibitisha amejiandikisha katika madarasa ambayo yanatimiza matakwa ya kuhitimu na yatatayarisha mtoto wako kwa ajili ya elimu zaidi ya shule ya sekondari, jeshi au kazi.
- ☐ Uliza mshauri wa mtoto wako ikiwa shule ya sekondari inatoa chaguo za ufundi kwa darasa la 10, ikiwa unataka.
- ☐ Jadiliana na mtoto wako kuhusu mpango unaowezekana wa kuweka akiba ya fedha kwa ajili ya chuo kikuu, ikiwa hujafanya hivyo.
- ☐ Zungumza na mtoto wako kuhusu raghba za kazi (Onet.org/miproximopaso.org) – pacareers.org
- ☐ Pata maelezo ya misingi ya gharama, kuweka akiba, na msaada wa kifedha.
- ☐ Himiza mtoto wako kujihusisha katika shughuli za ziada ambazo zinasaidia raghba yake na kujenga ujuzi wa maisha kama vile uongozi, kujitegemea, ubunifu, ushirikiano, kufanya maamuzi, na ujuzi wa kifedha.

**Darasa la 10**

- ☐ Kuwa na mkutano na mshauri wa shule ya mtoto wako ili kuhakikisha kwamba anafuata ratiba ya kuhitimu.
- ☐ Fanya utafiti kupitia intaneti au mkataba wa umma ili kupata maelezo ya mipango ya chuo/shule ya kiufundi, mafundisho binafsi, na gharama, na msaada wa masomo.
- ☐ Kumbusha mtoto wako kuendelea kuhudhuria madarasa ambayo yanatimiza matakwa ya kuhitimu na kujenga ujuzi.
- ☐ Endelea kuhimiza mtoto wako kujihusisha katika shughuli za ziada au za kujitolea.
- ☐ Himiza mtoto wako kutembelea chuo/shule za kiufundi na kushiriki katika mipango ya maandalizi ya chuo cha majira ya joto, ikiwa ipo.

**Darasa la 11**


- ☐ Fuatilia na mshauri wa shule ya mtoto wako ili kuhakikisha kwamba mtoto wako anafuata ratiba ya kuhitimu.
- ☐ Kumbusha mtoto wako kujiandikisha katika kozi zinazohitajika kwa ajili ya kuhitimu shule ya sekondari na/au kazi anayotaka.
- ☐ Kumbusha mtoto wako kujiandikisha kufanya PSAT wakati wa majira ya majani kupukutika (ikiwa huna uhakika zungumza na mshauri wako.)
- ☐ Andika orodha ya chuo/shule za kiufundi na mipango ambayo inavutia mtoto wako.
- ☐ Fanya utafiti na upunguze shule zinazowezekana za chuo cha elimu/shule ya kiufundi, masomo na kazi na mtoto wako. Kumbusha mtoto wako kujiandikisha kwa SAT na/au ACT wakati wa majira ya kuchipua.
- ☐ Kumbusha mtoto wako kujiandaa kwa SAT au ACT. Zungumza kuhusu umuhimu wake (jinsi matokeo yanaweza kuwaathiri katika kuingia kwenye chuo na kwa ajili ya msaada wa masomo.
- ☐ Himiza mtoto wako kuendelea kuchunguza na kufanya maamuzi kuhusu masomo na kazi.
- ☐ Endelea kuhimiza mtoto wako kutembelea chuo/shule ya kiufundi mwaka mzima. Kuwa na ufahamu wa safari za chuo ambazo shule ya mtoto wako inaweza kutoa.
- ☐ Andika orodha ya angalau vyuo vya elimu/shule za kiufundi tano ambazo zinatoa kozi ya masomo ambayo mtoto wako anapendezwa. Kumbusha mtoto wako kujiandaa kwa SAT ikiwa anafikiri kuifanya katika darasa lake la mwisho, ikiwa inahitajika.
- ☐ Endelea kufahamisha kuhusu misaada ya kifedha na kuzungumza na mshauri kuhusu mwongozo wa mtoto wako. Msaidie mtoto wako kutafuta msaada wa masomo ambayo yanalingana na mahitaji yako ya kifedha.
- ☐ Himiza mtoto wako kupanga shughuli za majira ya joto: kujitolea, kuhudhuria mipango ya majira ya joto, au kupata kazi au usanifu unaofanana na raghba yake na hujenga ujuzi muhimu.
- ☐ Wakati wa majira ya joto nenda kwenye safari za chuo kikuu za raghba za mtoto wako.

**Darasa la 12**

- [ ] Panga mkutano na mtoto wako na mshauri wa shule ili kuhakikisha kwamba anafuata ratiba kwa ajili ya kuhitimu.
- [ ] Punguza orodha ya vyuo/shule za kiufundi ambazo mtoto wako anapendezwa.
- [ ] Kumbusha mtoto wako kukamilisha na kuwasilisha maombi yote ya chuo.
- [ ] Kumbusha mtoto wako kuandika insha za maombi ikiwa inahitajika na fanya mwalimu apitie.
- [ ] Kumbusha mtoto wako kuwasilisha hati zote zinazohitajika kwa ajili ya msaada wa kifedha na usaidizi na/au misaada ya masomo iliyopo. (Wasilisha maombi ya FAFSA na PHEAA. Siku ya kwanza ambayo FAFSA inapatikana ni mnamo Octoba 1, studentaid.ed.gov)
- [ ] Msaidie mtoto wako kuunda kalenda ambayo inaonyesha tarehe muhimu na muda wa mwisho.
- [ ] Ikiwa barua za mapendekezo zinahitajika, kumbusha mtoto wako kuziomba angalau wiki nne kabla ya tarehe ya mwisho ya maombi.
- [ ] Kumbusha mtoto wako kujiandikisha kufanya SAT au ACT ikiwa inahitajika.
- [ ] Panga mkutano na mshauri wa mtoto wako ili kuhakikisha kwamba nakala za shule ya sekondari ziliwasilishwa kwa vyuo ambavyo matoto wako amejiandikisha (Novemba-Machi).
- [ ] Kumbusha mtoto wako kutoa nakala ya hati zote ambazo yeye hutuma na mfanye afuatilie na shule ili kuhakikisha kwamba amepokea maombi aliyoyaomba.
- [ ] Linganisha vifurushi vya usaidizi wa fedha kwa makini. Ikiwa unahitaji msaada, zungumza na mshauri wako au mfanyakazi wa MEP.
- [ ] Ikiwa huko tayari, tembelea chuo cha elimu/shule ya ufundi ambayo mtoto wako amechagua kabla ya kukubali.
- [ ] Angalia barua za mtoto wako za kukubaliwa au kukataliwa, kwa kawaida hutumwa kabla ya mwezi wa Mei.
- [ ] Hakikisha kwamba masomo ya ziada na karo ya mtoto wako zimelipwa.
- [ ] Hitimisha mpango wa nyumba na chakula kwa ajili ya mtoto wako.
- [ ] Tayarisha mtoto wako kwa ajili ya safari ya kusisimua.

## Kulipia Elimu ya Baada ya Sekondari

Kama inavyoonekana katika chati ya mtiririko, kuna aina mbili msingi ya msaada wa kifedha: zawadi (ruzuku na misaada ya masomo) na kujisaidia (mikopo au kazi-masomo). Mtoto wako anaweza hitaji zote. Anaweza kuhitaji msaada wako wa kifedha kulingana na msaada ambao anaopokea. Masharti haya yanaelezewa baada ya chati ya mtiririko.




### Maneno msingi

**Mikopo ya Moja kwa Moja ya Serikali:** Mpango ambao hutoa mikopo ya riba ya chini kwa wanafunzi wa elimu ya baaada ya sekondari na wazazi wao.

**Ruzuku ya Pell ya Serikali:** Msaada kutoka kwa serikali ya Marekani wa wanafunzi ambao wanahitaji kulipia chuo.

**Msaada wa Kifedha:** Msaada wa kifedha kutoka kwa serikali kuu wa kusaidia kulipia gharama za elimu katika vyuo vinavyotihimu vya elimu na shule ya kusomea kazi.

**Rukuzu:** Msaada wa kifedha, mara nyingi hutegemea hitaji la kifedha na msaada huo haupaswi kulipiwa.

**Mikopo:** Pesa ambazo wanafunzi wa chuo cha elimu cha na wazazi wao hukopa ili kusaidia kulipa chuo.

**PHEAA:** (Shirika la Msaada wa Elimu ya Juu ya Pennsylvania) hutegemeaa hitaji la kifedha.

**Mikopo za Ziada:** Mikopo kutoka kwa taasisi za kibinafsi zinapatikana ili kulipia gharama za chuo, kulingana na historia yako ya mkopo.

**Mikopo ya Wanafunzi Binafsi:** Mikopo kutoka kwa taasisi ya kibinafsi inapatikana kulipa gharama za chuo, kulingana na historia yako ya mkopo.

**Misaada ya Masomo:** Fedha zinazopewa mwanafunzi wa chuo kwa sababu ya mafanikio, uwezo, au historia maalum.

**Mikopo ya Ruzuku:** Inategemea hitaji la kifedha. Serikali hutoa ruzuku (hulipia) riba ya mkopo wakati mwanafunzi yuko shuleni na kwa kipindi cha nyongeza cha miezi sita baada ya kuhitimu.

**Mikopo isiyo ya Ruzuku:** Mikopo isiyotegemea hitaji ka kifedha. Mtoto atadaiwa riba kutoka wakati unapokopa pesa hadi wakati mkopo utalipwa.


**Kazi-Masomo:** Kazi inayotolewa kupitia chuo na kufadhiliwa na serikali ili kusaidia wanafunzi kulipia chuo kikuu.

Kwa maelezo kuhusu mipango ya msaada wa mwanafunzi, ikijumuisha kiwango cha juu cha fedha cha kila mwaka na viwango vya riba ya mkopo, tembelea www.*StudentAid.gov/parent*.


## Kuna faida gani kwa mtoto wako kuendelea na elimu ya baada ya elimu ya sekondari?

Je, mtoto wako anafikiria kuondoka shuleni ili kuingia kazini, ili aweze kuchangia katika gharama za familia yako? Uamuzi huu una matokeo makubwa kwa siku zijazo za mtoto wako! Zungumza wazi kuhusu wasiwasi wako na mshauri wa shule ya mtoto wako, mwalimu aliyeaminika, na wafanyakazi wa PA-MEP.
Watakusaidia kuchunguza njia mbadala.

Chati (inayopatikana hivi majuzi) inaonyesha kwamba elimu zaidi husababisha mapato ya juu. Mwanafunzi ambaye anahitimu kutoka shule ya sekondari huenda atapata zaidi kwa wiki kuliko mwanafunzi asiyekuwa na diploma ya shule ya sekondari, hasa katika kipindi cha maisha yake. Hii inathibitisha kuwa uamuzi wa kuondoka shule ya sekondari ili kufanya kazi huwa na matokeo makubwa.




## Njia za kutoka Shule ya Sekondari hadi Kufanya kazi




Kuna njia nyingi za mtoto wako kutoka shule ya sekondari hadi kufanya kazi. Inaweza kuwa yenye mpangilio au kuchukua hatua tofauti anapoendelea.

## Maombi ya Bila Malipo kwa Msaada wa Serikali kwa Mwanafunzi (FAFSA)

FAFSA ni ombi la kawaida linalotumika kuomba msaada wa kifedha kutoka kwa miradi yote ya serikali. Mchakato wa maombi haulipishwi na fomu inapatikana mtandaoni. FAFSA ni muhimu kwa mtoto wako kupokea misaada, kazi ya utafiti, mikopo, na hata baadhi ya misaada ya masomo.

Wazazi wanaweza pia kuunda Mpango wa Kuweka Akiba wa Chuo cha Elimu wa 529 - Wazazi wanaweza kuanza kuweka akiba ya fedha kupitia mwajiri wao au taasisi ya kifedha. Mpango wa 529 ni mpango wa akiba wa kupunguziwa kodi ulioundwa kuhamasisha kuweka akiba kwa ajili ya gharama za elimu ya baadaye. Mipango ya 529, inayojulikana kisheria kama "mipango
inayostahili ya masomo," inafadhiliwa na serikali, mashirika ya serikali, au taasisi za elimu na inaruhusiwa na Sehemu ya 529 ya Kanuni za Mapato ya Ndani. Unaweza kutumia mpango wa 529 kulipa gharama za elimu zaidi zilizostahili katika vyuo vingi vya elimu na vyuo vikuu, na shule nyingi za kiufundi na kufundisha kazi. Mpango wa Kuweka Akiba wa Chuo cha 529 cha Pennyslvania hutoa mipango miwili ya kuweka akiba. Mpango wa Uwekaji Akiba Uliohakikishiwa wa PA 529 (GSP) ni mpango wa kupunguza hatari ambao husaidia akiba yako kuendana na mafundisho zaidi ya elimu. Mpango wa Uwekezaji wa PA 529 (IP) hukuruhusu kuchagua kutoka kwa machaguo 16 ya uwekezaji kutoka kwa Kikundi cha Vanguard. Hakuna kimo cha mapato, na mtu yeyote anaweza kuchangia. Kwa maelezo zaidi, nenda kwa https://www.pa529.com.

## Misaada ya Masomo

Misaada ya masomo ipo kwa kila mwanafunzi anayetafuta elimu ya chuo. Baadhi ya misaada ya masomo inajumuisha: ya kitaaluma, ya riadha, ya kikundi fulani cha umbari, ya wanawake, na huduma ya jumuiya, miongoni mwa zingine. Mambo ya ziada ya kufanya maombi yako ya msaada wa masomo kuwa tofauti ni:

- Saa za kujitoleoa
- Kujiandikisha kwenye klabu ya shule
- Kuwa unahusika zaidi shuleni
- Kuwa unahusika zaidi katika jumuiya

# Vidokezo na Rasilimali za Ziada